**MTIHANI WA TATHMINI YA ENEO GATUZI LA NANDI MASHARIKI, TINDERET NA NANDI KUSINI 2016**
**KISWAHILI**
**INSHA**
**102/1**
**KARATASI LA KWANZA**

1. Andika barua kwa mhariri wa gazeti la "Mwangaza" ukiangazia sababu na madhara ya udanganyifu katika mitihani ya kitaifa nchini.
2. Vita vinavyoendelezwa na Serikali ya Kenya dhidi ya magaidi nchini Somalia vimeleta faidi nchini. Jadili.
3. Tunga kisha kinachothibitisha ukweli wa methali hii:
   Mchuma janga hula na wa kwao.
4. Andika insha itakayoishia kwa:
   …………… alipohitimisha hotuba yake wanafunzi wote walikuwa wamepata mwanga kuhusu madhara ya mihadarati.

**MTIHANI WA TATHMINI YA ENEO GATUZI LA NANDI MASHARIKI, TINDERET NA NANDI KUSINI 2016**
**KISWAHILI**
**102/2**
**LUGHA**
**KARATASI LA PILI**

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Waziri wa uchukuzi Bwana Msafiri ametoa mwto kwa kila mwananchi kusingatia sheria za barabarani ili kumaliza visa vya ajali vilivyokithiri. Alisema kuwa ongezeko la ajali za barabarani linachangiwa pakubwa na watu binafsi.

Akiongea katika hafla ya kuzindua mbinu za kuhakikisha usalama barabarani, Bwana Msafiri alisema yasikitisha kuona kuwa ajali za barabarani zimeongezeka katika siku za hivi majuzi. Alielezea kuwa wizara yake imekerwa na utekelezaji wa majukumu na mapuza miongoni mwa wanaohusika na sekta ya uchukuzi.

Alisema wengi wa wenye magari wamepuza masharti mengi ambayo yaliwekwa na wizara, yaliyokusudiwa kugunguza ajali. Alisema magari mengi yamekuwa kachara na kwamba mengi yameng'olewa vidhibiti mwendo. Basi magari yanaendeshwa kwa kasi ya umeme. Hili limeongeza ajali kwa kiasi kikubwa. Mengi hayana mishipi ya usalama na wasafiri hukabiliwa na hatari wanaposafiri. Aliongeza kuwa sura ya magari hayo ni dhihirisho kuwa wenye magari wamepotoka kabisa, "magari mengi yamerembeshwa hata kwa picha chafu, jambo linalodhihirisha utovo wa mbeko na kutofuata sheria. Mengine yanacheza muziki kwa sauti ya juu hivi kwamba hata dereva na utingo hawawezi kusikia grudumu liking'oka. Baadhi yao yanaonyesha picha chafu chafu za video na kuufanya usafiri kuwa vyumba vya sinema chafu!" Alisema kutovaa sare kwa madereva na makondakta na kuwapakia abiria kupita kiasi ni kilele cha upuui wa sheria zilizowekwa.

Wasafiri pia wanapuuza masharti yaliyowekwa kwa lengo la kuwafaa, "alisema waziri. Alisikitika kuwa wasafiri wengi hawafungi mishipi ya usalama hata inapopatikana, aidha wanakubali kuingia magari yaliyojaa tayari, hali inayoongenzea uwezekano wa gari kupata ajali kwa kulemewa na uzito. Aliwakumbusha kuwa gali likipata ajali wakiwa wamepakiwa hivi, hawezi kugharamiwa na bima ya gari kwa vile bima yenyewe hukatiwa idadi mahususi ya wasafiri. Aliwalaumu watembeaji barabarani kwa kutozingatia sheria za kawaida. Alisema kwa mfano katika gurufu kuna mahali ambako kuna vivuko ila hawavitumii na wengine huishia kugongwa na magari.

Mwisho aliwalaumu maafisa wa trafiki wanaotekeleza majukumu yao. Akitisha kuwachukulia hatua kali, alisema kuwa yaskitisha kusikia kuwa wanachukua kadhongo na kuyaachilia magari yaliyo na kasoro badala ya kuyashtaki kulingana na sheria. Aliwaongezea lawama wasafiri kwa kunyamaza wanapoyaona haya yakitendeka machoni. Alisababisha kicheko aliposema kuwa baadhi ya wasafiri huwahimiza makondakta watoe chai haraka ili waendelee na usafiri ya bila kujali hatari wanazojiingiza kwazo.

Akionya kuwa angechukua hatua ya kuregesha utulivu, alihitimisha kwa kusema kuwa wizara yake limetoa ilani kwa watumiaji wote wa barabarani. Alitoa makataa ya siku kumi na nne ambapo yoyote asiyefuata kaida zote za barabarani atachukuliwa hatua kisheria.

**Maswali**

a) Fafanua sababu za mwito wa waziri wa uchukuzi Bwana Msafiri? (alama 2)
b) Eleza jinsi wenye magaari wamechangia katika kukithiri kwa visa vya ajali barabarani? (alama 4)
c) Fafanua mchango wa wasafiri katika kudorora kwa hali ya usalama barabarani. (alama 3)
d) Eleza majukumu ya maafisa wa trafiki katika kudumisha usafiri kulingana na ufahamu. (alama 3)
e) Toa visawe vya maneno yafuatayo. (alama 3)
   (i) Kondakta:……………..……………………………………………………………..
   (ii) Toa ilani:……………..……………………………………………………………..
   (iii) Toa makataa:……………..……………………………………………………………..

for more free revision papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

2. **UFUPISHO: (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Serikali kupitia Wizara ya Elimu imetoa mwongozo wa karo ambao unastahili kuzingatiwa katika shule za upili kufuatia haua ya shule mbalimbali kuongeza karo kwa viwango mbalimbali. Hatua hiyo inadhamiriwa kumking mzazi dhidi ya kunyanyaswa kifedha walimu hasa ikizangiwa kuwa gharama ya maisha imepanda mara dufu.

Hata hivyo, ingekuwa bora ikiwa serikali ingefanya maamzi kwa ushirikiano na walimu wakuu maana kwa hakika suala la karo linahusu matumizi ya fedha ambayo pia huja na gharama zake. Gharama hii inaokana na ununuzi wa vitabu vya Kada na vya mazoezi, karatasi za uchapishaji mitihani, kwa kuwa wanafunzi sharti wasome na waandike.

Vilevile, gharama hii inatokana na ununuzi wa kemikali za kutumiwa katika maabara. Aidha kuna gharama ya kuendesha michezo na tamasha za muziki na drama. Wanafunzi wa shule za malazi hula na kulala na kwa sababu hiyo maamuzi ya kifedha lazima yafanywe.

Jambo ambalo linastahili kuangaliwa kwa makini ni viwanga vya kupanda kwa gharama ya maisha. Lazima tujiulize gharama hiyo imepanda kwa kiasi gani na wapi? Kwa kweli haiwezekani kununua kilo moja ya mahindi kwa bei hiyo hiyo Kitale, Mombasa na Turkana. Vile vile ni muhimu kujiuliza ikiwa shule husika ni ya mashambani au ya mjini? Kwa hivyo sharti la kifedha ni muhimu katika kuamua karo ya shule na maeneo mbalimbali nchini.

Pili, hebu tuangalie ikiwa shule inavyohusika ni ya kiwango cha kaunti ndogo, kaunti au cha kitaifa. Hili ni muhimu kwa kuwa hali ya masomo katika shule hizo hutofautiana. Tofauti kuu hutokana na miundomisingi na programu za masomo zinazoendeshwa.

Kwa mfano, programu za kitahmini, kompyuta na zinazohusu ziara huhitaji fedha nyingi. Shule ambayo ina masomo kama vile muziki, sanaa na sayansikimu sharti zitoze karo ya juu kwa kuwa masomo hayo huandamana na gharama ya kununua vyombo na vyakula?

Sasa mbona fedha za ziada? Wanaotetea kupunguzwa kwa karo wana punguza mchango wa motisha katika ufanifu wa masomo. Ndio, baadhi ya shule hutoza karo ya juu ili kuwamotisha walimu kwa vyakula na kwa zawadi ili kuwastahi wanapopata matokea mema. Hali hiyo huwafanya kujikakamua kazini na kutoa huduma ya hali ya juu.

Fedha za ziada vile vile, hutumiwa kuwajiri walimu wa ziada ikizingatiwa kuwa serikali haijawaajiri walimu wa kutosha. Pia katika baadhi ya shule, wanafunzi huandaliwa vyakula spesheli tofauti na mseto wa maharagwe na mahindi almarufu 'maram' uliozoeleka katika shule nyingi ikumbukwe kuwe lishe bora ni mojawapo ya haki za kimsingi kwa watoto ambayo sharti iheshimiwe.

Kwa marefu na mafupi yake, serikali haipaswi kuweka viwango sawa vya karo kwa kila shule kwa maana hilo huenda likazua mgogoro wa kiutawala katika shule nyingi. Shinikizo za kupunguzwa kwa karo inayotozwa hasa katika shule za upili zinafaa kutetewa kimantiki wala si kihisia.

Mambo huenda yangekuwa tofauti ikiwa serikali ingewajibika kwa upande wake kwa kuwaajiri walimu wa kutosha kuwaongeza walimu mshahara na kuwatambua kwa zawadi wanapofanya kazi nzuri na kuwapandisha vyeo. Hata hivyo, mgala muue na haki umpe; hatua kali zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya walimu wanaowatoza wazazi karo ya juu kupindukia ili kuendeleza maslahi yao ya kibinafsi.

Naamini kuwa hatua ya Waziri wa Elimu kukutana na washikadau katika sekta ya elimu kuhusu karo na uteuzi wa wanafunzi wa kujiunga na shule za upili ni ya busara na inafaa kuta mwelekeo mzuri kuhusu masuala tata yaliyopo kwa sasa.

***(Makala kutoka gazeti la Taifa Leo, January 8, 2016)***

(a) Fafanua mambo muhimu yanayostahili kuzingatiwa katika kutathmini viwango vya karo katika shule nchini Kenya. (Maneno 65 – 70) (alama 8, 1 ya mtiririko)

(b) Fupisha aya tatu za mwisho.(maneno 40 – 45) (alama 7, 1 ya mtiririko)

**MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Ukizingatia sehemu ya kutamkia, mwinuko wa ulimi na hali yam domo, tofautisha sauti zifuatazo. (alama 3)
/ *e* /, / l / na / u / ……………………………………………………………………………………

(b) Ukitolea mfano eleza aina **mbili** za miundo ya silabi katika Kiswahili. (alama 2)

(c) Eleza maana ya mghuno katika lugha ya Kiswahili. (alama 1)

(d) Kwa kutolea mfano mwafaka, fafanua tofauti iliyopo kati ya kishazi na kirai. (alama 2)

(e) Ukitolea mfano mwafaka, fafanua majukumu yoyote **manne** ya viambishi awali. (alama 2)

(f) Nomino zifuatazo zinapatikana katika ngeli zipi? (alama 1½)

for more free revision papers visit : www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

i) Chumvi:………………………………………………………………………………
ii) Nywele:…………………………………………………………………………....
iii) Mafuta:……………………………………………………………………………..

(g) Eleza matumizi ya kiambishi 'ku'
Kulia kwake kulisababisha msongamano wa watu alikokuwa. (alama 1½)

(h) Tunga sentensi yenye muundo wa:
N + V + T + H + N + E + U + T. (alama 4)

(i) Yakinisha katika umoja: (alama 2)
Msingalivumilia nyakati ile msingalipata zawadi kubwa.

(j) Andika katika udogo.
Jijipu lilipasuka lenyewe. (alama 1)

(k) Ukitolea mfano fafanua njia zozote **tatu** zinazotumiwa katika uunjdaji wa maneno. (alama 3)

(l) Ukitungia sentensi, onyesha matumizi ya vivumishi vya nomino. (alama 2)

(m) Tunga sentensi kubainisha matumizi ya vivumishi vya nomino katika ngeli ya U – I; katika umoja na wingi. (alama 2)

(n) Ukitolea mfano mwafaka, eleza tofauti iliopo katika kauli zifuatazo.
Kutendeana na kutendana. (alama 2)

(o) Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Mwamburi alitumia ufunguo kumfungulia Rashid mlango.

(p) Andika katika usemi wa taarifa:
"Nataka ufikirie sana juu ya maisha yako ya ndoa. Sitaki uishi maisha yasiyo na mweleko." Babu alinishauri.(alama 3)

(q) Kwa kutoa mfano, eleza matumizi mawili kila mojawapo wa alama zifuatazo:
i) Ritifaa
ii) Kama kituo

(r) Eleza maana ya msemo ufuatao :
Kula kitana. (alama 2)

3. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a) Eleza maana ya lugha rasmi. (alama 2)
b) Fafanua sifa zozote za lugha rasmi. (alama 8)

for more free revision papers visit : www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479